# JKT LEO

JARIDA LA MTANDAONI LA JESHI LA KUJENGA TAIFA

TOLEO NA. 186 19 JUNI, 2022


# KATEKELEZENI MAJUKUMU YENU WAKATI WA VITA NA AMANI - MHE. DKT STARGOMENA TAX



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax akihutubia Wahitimu wa Kozi ya Ukamanda na Unadhimu-Duluti baada ya kufunga Kozi hiyo.


Imetolewa na Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,
Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sanduku la Posta 2963, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 2962078. Nukushi: +255 26 2962080
Barua pepe: info@jkt.go.tz Tovuti: www.jkt.go.tz

# KATEKELEZENI MAJUKUMU YENU WAKATI WA VITA NA AMANI - MHE. DKT STARGOMENA TAX

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb), Amewataka wahitimu wa kozi ya Ukamanda na Unadhimu (CSC) kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuzikabili changamoto watakazokutana nazo wakati wa amani na vita.

Mheshimiwa Dkt Tax amesema hayo wakati wa mahafali ya kufunga kozi ya kundi la 36 na Mahafali ya kwanza kwa masomo ya Ulinzi na USalama 2021/22 ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo cha kijeshi (CSC) Duluti kilichopo jijini Arusha.

Amefafanua kuwa, Kozi hiyo inafanyika nchi mbalimbali Duniani kote na mafunzo yanayotolewa hayana tofauti kwani lengo la kuwafanya Maafisa wanaohudhuria kozi hiyo kuwa na moyo wa kujiamini sambamba na kutatua changamoto zinazowakabili wakati wa vita na wakati wa amani.

Aidha, Mhe. Tax amewapongeza Wahitimu husani Maafisa Wanawake kwa idadi yao kubwa ya kuhudhuria kozi hiyo, Sambamba na kuwataka wanawake nchini kuendelea kujiunga na Jeshi.

" Wanawake nchini wasisiste kujiunga na Jeshi na mara wapatapo nafasi watumie bidii na Weredi mkubwa katika mafunzo bila kujali jinsia zao. "ameongeza Mhe. Dkt. Tax

Amesema, anafahamu kuw kazi ya Jeshi ni ngumu sana ila unapoamua kujiunga huna budi kuweka jinsia pembeni na kuwa Mwanajeshi sambamba na kufanya yote yanayotakiwa kufanywa na mwanajeshi wakati wa mafunzo.

Nae, Mkuu cha Chuo cha Ukamanda na Unadhimu - Duluti, Brigedia Jenerali Sylvester Ghuliku amesema katika muda wa masomo wahitimu wamefundishwa kozi ya Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Astashahada na shahada ya uzamili ili kukabiliana na matishio ya Ulinzi na Usalama kwenye nchi zao.

Kwa upande wake , Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele amewapongeza Wahitimu kutoka JKT na kuwatakia mafanikio katika utendaji kazi pindi watakaporudi katika maeneo yao ya kazi.

Kwa niaba ya wahitimu Wa kozi hiyo kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Luteni Kanali Leah Mtuma aliwahasa Wanajeshi wanawake wafanye mitihani na kupata sifa ya kujiunga na chuo hicho kwani mitihani ni ya kawaida na pindi wanapopata nafasi ya kuchaguliwa chuoni hapo wasisite kujiunga.

Akielezea siri ya kuwa Mwanafunzi Bora (Best Student) katika kozi hiyo Meja Mugisha Bukagile ambaye anahudumu JKT idara ya Tehama amesema siri kubwa ni ushirikiano kutoka kwa wahitimu wenzake pamoja na jitihada binafsi.

"Siwezi kujisifia bali jitihada binafsi na ushirikiano wa wanafunzi wenzangu na wakufunzi umenifanya niwe mwanafunzi bora lakini kikubwa ni nidhamu na kutekeleza majukumu unayopewa kwa wakati". Meja Bukagile.

Kozi ya Ukamanda na Unadhimu kundi la 36, 2021/22 ilianza tarehe 19 Julai 2021 na kufungwa tarehe 18 June 2022 ikiwa na Wanafunzi 68 na kufanikiwa kumaliza wanafunzi 67 ikiwa na Maafisa Wanawake idadi 16 na Maafisa wanaume idadi 51 huku Mwanafunzi mmoja akifariki kwa ugonjwa.

Kozi hiyo ilihudhuriwa pia na Wanafunzi kutoka Mataifa mbalimbali ikiwemo nchi za Uganda, DR Congo, Misri, Uswatini, Kenya, Bangladesh, Malawi, Mozambique, Nigeria, Rwanda na Uganda.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) akisaini kitabu cha wageni katika Chuo cha Cha Ukamanda na Unadhimu Duluti wakati wa mahafari ya kufunga kozi katika Chuo hicho Jijini Arusha.



Mkuu wa chuo Cha Ukamanda na Unadhamu CSC Brigedia Jenerali Sylvester Ghuliku akitoa Neno kwa wahitimu na Wageni waalikawa katika Hafla ya Mahafali ya chuo cha Ukamanda na Unadhimu- Duluti Arusha.



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax akikabidhi zawadi kwa mshindi wa jumla Luteni kanali Shohan Khan wa Bangladesh katika kipengele cha wanafunzi wa mataifa ya nje.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax akikabidhi cheti kwa Luteni kanali Fatuma Makame wakati wa mahafali ya kufunga kozi ya Ukamanda na Unadhimu Duluti Arusha





Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) akikabidhi cheti kwa Mkurugenzi wa Ukaguzi Ndani JKT Luteni Kanali Hillary Kabandika wakati wa mahafali ya kufunga kozi ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo hicho.

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) akimkabidhi cheti Mwanafunzi Bora (Best Student) Meja Mugisha Bukagile kutoka JKT.



# MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) akimkabidhi cheti Meja Lucy Batakanwa wakati wa mahafali ya kufunga kozi ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo hicho.





Baadhi ya Wahitimu wa Kozi ya kundi la 36 wa Mafunzo ya Ulinzi na Usalama 2021/22 ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo cha kijeshi (CSC) Duluti kilichopo jijini Arusha wakifuatilia sherehe za ufungaji wa mafunzo hayo.

Baadhi ya Wahitimu wa Kozi ya kundi la 36 wa Mafunzo ya Ulinzi na Usalama 2021/22 ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo cha kijeshi (CSC) Duluti kilichopo jijini Arusha wakifuatilia sherehe za ufungaji wa mafunzo hayo.



# MATUKIO KATIKA PICHA




**Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele akiwa katika picha ya Pamoja na Wahitimu wa Kozi ya kundi la 36 wa Mafunzo ya Ulinzi na Usalama 2021/22 ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo cha kijeshi (CSC) kutoka JKT.**



**Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele akimpongeza Kamanda Kikosi cha Mgambo JKT Luteni kanali Geofrey Mvula kwa kumaliza kozi ya Ukamanda na Unadhimu wakati wa Mahafali ya kumaliza kozi hiyo.**



**Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) akiambatana na Mnadhimu Mkuu wa JWTZ Luteni Jenerali Methew Mkingule (kushoto) na Mkuu wa Chuo Cha Ukamanda na Unadhamu CSC Brigedia Jenerali Sylvester Ghuliku.**

# MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb), akiwa katika picha ya pamoja na Wahitimu wa Kozi ya kundi la 36 wa Mafunzo ya Ulinzi na Usalama 2021/22 ya Ukamanda na Unadhimu kutoka Chuo cha Kijeshi (CSC) Duluti kilichopo jijini Arusha.







Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mnadhimu Mkuu wa JWTZ Luteni Jenerali Methew Mkingule (kulia kwake) na kushoto kwake ni Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Duluti Brigedia Jenerali Silvester Ghuliku na Maafisa wanawake waliomaliza kozi hiyo wakati wa mahafari ya kufunga kozi ya ukamanda na unadhimu katika chuoni hapo.

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt Stargomena Tax (Mb) (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mnadhimu Mkuu wa JWTZ Luteni Jenerali Methew Mkingule (kulia) na kushoto kwake ni Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Duluti Brigedia Jenerali Silvester Ghuliku na Makamanda pamoja na wawakilishi kutoka nchi za nje wakati wa mahafali ya kufunga kozi ya Ukamanda na Unadhimu katika chuo hicho.

